

HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA

MKOTOKUYANA SEKONDARI,
S.L.P 49,
NACHINGWEA.

Kumb. Na. MKSS/M/J.21/04

10/12/2020

MZAZI / MLEZI WA _____
S/M _____

YAH: TAARIFA YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKOTOKUYANA KIDATO CHA KWANZA 2021

Husika na somo la hapo juu.

Ninafurahi kukufahamisha kwamba mwanao ni miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari Mkotokuyana kidato cha kwanza 2021.

Aidha nampongeza kwa kupata nafasi hii adimu ambayo wengine walitamani ila wamekosa.

Shule ya sekondari Mkotokuyana ipo katika kata ya Mkotokuyana, kijiji cha Mkotokuyana. Ni shule ya kutwa na mwanafunzi atajigharamia kwa usafiri wa kwenda na kurudi nyumbani.

Sare za shule:

Wasichana

1. Awe na sketi mbili rangi ya kahawia
2. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
3. Viatu jozi mbili vyeusi vya kufunika miguu vyenye gidamu (kamba)
4. Soksi nyeupe jozi mbili
5. Vifaa binafsi vya michezo (tisheti na traki) rangi ya bluu
6. Anaweza kuwa na hijabu

Wavulana

1. Suruali mbili ndefu zisizo za kubana (modal) rangi ya kahawia
2. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
3. Viatu jozi mbili vyeusi vyenye gidamu (kamba)
4. Soksi nyeupe jozi mbili
5. Raba kwa ajili ya michezo
6. Vifaa vya michezo (tisheti na bukta) rangi ya bluu

Mahitaji mengine kwa wote

1. Fagio ya mnazi (chelewa) kwa ajili ya usafi
2. Aje na fyekeo moja (jipya) na liwe limenolewa

VIFAA:

Vitakaguliwa pindi mtoto anaporipoti shuleni na vikikabidhiwa itakuwa ni mali ya shule.

1. Aje na daftari 10 counter book (quire 2 au 3)
2. Ruler
3. Mathematical set (mkebe)
4. Kalamu ya wino
5. Awe na begi la kubebea daftari
6. Kamusi ya Kiingereza – Swahili
7. Faili moja la plastic (kwa ajili ya kutunzia mithani)
8. Rimu moja (1) A4 ya karatasi)

Afya ya mwanafunzi ni jukumu lako mzazi/mlezi hivyo inafaa mwanao akajiunga na CHF ila huduma ya kwanza inapatikana shuleni, chakula cha mchana ni jukumu lako mzazi/mlezi ambacho utajulishwa kiasi cha kuchangia na namna ya uchangiaji siku ya kikao cha wazazi.

Kumbuka kwamba Elimu ni bure. Hivyo mwandae mwanao mapema ili aweze kupata Elimu ya Sekondari.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 mzazi/mlezi unatakiwa kuripoti na mwanao siku hiyo bila kukosa muda wa saa 1:30 asubuhi.

Zingatia agizo hili.

"ELIMU NI CHANZO CHA MAENDELEO"

Karibu sana shule ya Sekondari Mkotokuyana

Kwa mawasiliano zaidi 071962433 / 0718553640

Ahsante.

.....
SANGA R. F
MKUU WA SHULE

NACHINGWEA DISTRICT COUNCIL

MKOTOKUYANA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 49,
NACHINGWEA.

10/12/2020

TO THE MEDICAL OFFICER

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR

Please examine the above named pupil and give us a report regarding his. Her suitability for under taking Secondary School Studies.

1. Blood _____
2. Stool _____
3. Tb test _____
4. Syphilis test _____
5. Urine examination _____
6. Eye test _____
7. Ears test _____
8. Chest _____
9. Spleen _____
10. Abdomen _____
11. Pregnancy (for girls only) _____

ANY ADDITIONAL INFORMATION: E.g. physical disability, or impairment, infection, family diseases and any special care.

I certify that the above is **FIT/UNFIT** for undertaking Secondary School studies, if UNFIT please give reason.

Name of **Medical Office** _____ Signature _____

Date _____ Official Stamp _____

Yours,

.....
THE HEADMASTER